**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA**

**BARAZA LA WATAALAM WA MAABARA**

# TANGAZO

## UHUISHAJI WA LESENI KWA KUZINGATIA ALAMA ZA CPD

Baraza la Wataalam wa Maabara linawatangazia Wataalam wa Maabara kuwa ifikapo tarehe 30 Septemba, 2024 muda ulioongezwa kwaajili ya kukamilisha alama za CPD kwa mwaka wa fedha uliopita (2023/2024), utafikia kikomo, sambamba na hilo Baraza linapenda kukumbushia mambo yafuatayo:

1. Wataalam kuhakikisha wanafikisha alama za CPD elekezi ili waweze kuhuhisha leseni zao kwa mwaka huu wa fedha 2024/2025. Aidha baada ya mwezi Septemba 2024 alama zote zilizopatikana katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 hazitatumika katika kuhuisha leseni, kwakuwa zitaondolewa katika akaunti zao.
2. Wataalam ambao wamelipia ada zao za mwaka 2024/2025 lakini bado hawajaidhinishwa (not approved) kwa sababu ya kutokufikisha alama za CPD zinazohitajika, wahakikishe wanazifikisha alama hizo na kufanya mawasiliano kwa namba **0734005777** ili waweze kuidhinishwa.( Aproved ).
3. Wataalam ambao waliomba "control number" kwenye mfumo wa HPRS na hawajafanya malipo, wanakumbushwa kufanya malipo hayo ili kuepusha namba hizo kuisha muda wake (get expired), ambayo husababisha usumbufu mkubwa sana.
4. Baraza litatoa kadi za uhuishwaji leseni (Licensing card) mwishoni wa mwezi wa Septemba,2024 na kuzisambasa katika Mikoa na Halmashauri, hivyo Wataalam mnaombwa kuhakiki taarifa zenu kwenye mfumo wa HPRS za sehemu mliopo sasa ili kadi hizo ziweze kuwafikia, Kadi hizo zitatolewa kwa Wataalam ambao wameidhinishwa (approved) katika kipindi cha mwezi Julai mpaka Septemba, 2024.
5. **Wataalam ambao watalipia baada ya kipindi hiki watafanya juhudi binafsi za kufuatilia kadi hizi katika Ofisi ya Msajili Dodoma-UDOM.**

**Imetolewa na**
Ofisi ya Msajili
Baraza la Wataalam wa Maabara
28.08.2024

HEALTH LABORATORY PRACTITIONERS COUNCIL
28 AUG 2024
P.O.Box 743
DODOMA